Teacher.co.ke

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
Kenya Certificate of Secondary Education

102/2
PDF Compressor Free Version

Karatasi ya 2

# KISWAHILI
## LUGHA
## Mar. 2022 – Muda: Saa 2½

Jina ............................................................ Nambari ya Mtahiniwa ............................

Sahihi ya Mtahiniwa ............................. Tarehe ..................................................

### Maagizo

(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(c) Jibu maswali **yote.**
(d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
(e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
(g) **Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.**
(h) **Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

© 2021 The Kenya National Examinations Council


915019

Geuza ukurasa

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**1. UFAHAMU** (Alama 15)

PDF Compressor Free Version

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Ulikuwa wakati wa jioni jua limepunguza udhia wake na **upepo mwanana ulikuwa ukipita na kuzipapasa ngozi zetu** mfano wa pamba. Kama ilivyokuwa desturi yetu hapo kijijini, siku hiyo pia tuliketi nje ya nyumba yetu tukafanya duara kulizunguka birika la kahawa. Kila mmoja alichukua glasi akajimiminia kiasi cha kahawa alichotaka na kurudi kuchukua mahali pake kitini.

Tulipotia fahamu tulipata mazoea haya yamekita mizizi nasi tukawa hatuna budi kuyakumbatia. Hatukuyakumbatia tu, bali tuliyakumbatia kwa dhati ya moyo. Vikao hivi havikuwa tu hazina kubwa kwetu bali pia vilikuwa vya thamani isiyomithilika. Hapa ndipo **tulinoleana bongo** kwa kupashana habari. Leo hii tumo katika kuzungumzia nguzo kuu za maendeleo, tena maendeleo ya haja ambayo yataibadilisha sura ya mwananchi na nchi. Nahodha wa kikao cha leo anampa msemaji wa kwanza nafasi naye hakusita kushika usukani.

"Nionavyo mimi, maendeleo yatawezekana ikiwa elimu itaweza kukidhi haja za watu. Sio nadharia tupu ambayo huwezi kuitumikiza ikaleta matokeo. Lazima nchi imwezeshe kila mtu kupata elimu ya msingi ambayo itamsaidia kufikia habari za kimsingi, iwe ni kupitia kwa magazeti au vitabu. Habari hizo zitamfunua macho, akaona na kuhakiki mambo. Wenzangu, jibu ni elimu! Maendeleo yanategemea elimu," kijana mmoja alisema kwa mhemko.

Muda wote huo kila mtu alikuwa ametulia. Wapo waliotikisa vichwa kukubaliana naye na wapo waliovitikisa kukataa. Hata hivyo, walikuwepo waliokaa tu kama mawe. Hawakuonyesha ishara yoyote ya kuguswa na maneno yale. Mwendesha mjadala alifanya ishara na mara kijana wa miraba minne aliyekuwa amevaa shati lililompwaya akasimama na kuzungumza kwa sauti nzito.

"Mtazamo wangu mimi bwana ni tofauti. Ukitazama duniani kote, kila nchi iliyoendelea imewekeza sana viwandani. Uzalishaji wa viwandani ndio dawa mjarabu. Hebu vuta fikra! Kila tunachotumia kuanzia kalamu, kitabu, nguo, msumari, saruji ... yaani kila kitu chenye nafasi katika maisha yetu kimepitia hatua za uzalishaji viwandani..."

"Si ndio hayo! Naona unaniunga mkono aisee! Viwanda huendeshwa kwa elimu au ukipenda maarifa. Na maarifa hayo huja kwa mafunzo ambayo ni elimu," alifafanua yule kijana wa kwanza.

"Nipe muda Sudi! Nipe muda nimalizie **hoja** yangu. Ninachosema ni kuwa elimu bila utumizi wake kuzalisha huduma na bidhaa muhimu haina nafasi kubwa katika maendeleo ya jamii. Elimu si mwisho wa yote bali mwanzo. Elimu inafaa kuzalisha. Na uzalishaji muhimu zaidi ni wa viwandani. Kwa hivyo, nionavyo mimi msisitizo mkubwa unafaa kuwa katika kutengeneza viwanda na kuvifanya kuzalisha."

Jama alimaliza mazungumzo yake akatulia na kupiga funda la kahawa. Hapo ndipo mwendesha mjadala alipompa kijana mwingine nafasi naye atoe maoni yake. Kijana huyo mdogo wa kimo na umbo alianza kusafisha koo huku wenzake wakimshangilia. Kwa kawaida kijana huyo alikuwa na mbwembwe nyingi.

"Bwana Spika," alianza huku wenzake wakishangilia kwa kila namna. Walipotulia aliendelea, "Mimi najua wapo watakaoniita mjinga hapa lakini naamini miundombinu ni muhimu zaidi. Watu hawawezi kuendelea bila mfumo mzuri wa barabara na reli, usambazaji wa kuridhisha wa umeme, viwanja vya kutosha na bora kwa ajili ya vijana kunoa vipawa vyao..."

Maneno yake yalifunikwa ghafla na kelele za kumshangilia na kumsifu huyu kijana waliyemwita Sumaku. Hii ilikuwa lakabu waliyompa kwa uwezo wake wa kuelewa mambo kwa wepesi na kwa kujua kuwavutia vijana wenzake maana alijua wapi pa kugonga ili gogo litoe mlio. Alipoona bado wanashangilia aliinua mkono wake wa kushoto juu na kusema, "Basi! Basi,

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

wananchi, sina shaka ujumbe umefika." Kisha aliketi na kuwaacha wenzake wakiumwa mbavu kwa vicheko.

PDF Compressor Free Version

Utulivu ulirejea taratibu. Kabla kila mmoja amakinike, mwendesha mjadala alimpa nafasi mzee mmoja aliyekuwa amevutwa na mazungumzo hayo naye kuchangia. Mzee yule alicheka kidogo, akasafisha koo na kuwapongeza wachangiaji waliomtangulia kisha naye akasema yake.

"Mambo hayo yote ni kama pacha lakini pekee hayatoshi. Miundomsingi inahitaji watu wa kuitumia, navyo viwanda vinahitaji wafanyakazi. Watu hao wasipokuwepo, vitu hivyo havina maana. Watu hao wanahitaji kuwa na afya bora. Hospitali zinahitaji kuwa katika kiwango cha kutoa huduma za kuridhisha. Zinahitaji wataalamu wasiobabaisha, vyombo vya kisasa vya udodosi na upasuaji, dawa nzuri na mazingira safi kwa ajili ya wagonjwa. Halafu huduma hiyo nzuri iwe inaweza kufikiwa na kila mtu."

Alitua kidogo. Sasa kila mtu alikuwa ametulia kama ardhi iliyonyeshewa. Kisha akaendelea, "Pamoja na hayo, ipo haja ya huyo mfanyakazi kupata pa kuweka ubavu wake. Akiisha kuichapa kazi anahitaji kurudi nyumbani. Si nyumbani kwa maana ya mahali pa kupangisha bali nyumbani kwa maana ya mahali pake mwenyewe. Hivyo panahitaji kuwepo mpango wa wafanyakazi kununua nyumba kwa bei nafuu. Mtu si kama ndege anayeweza kuishi mtini na akaamka kushika shughuli zake. Mtu huhitaji makao yake. Haya yote yakifanywa kwa pamoja na kwa ufanisi basi tutakuwa tumeanza kujiandaa kupaa kwa mbawa zetu wenyewe."

Alipomaliza kusema alishika njia na kwenda zake bila kutazama nyuma. Sote tulijikuta tunacheka kwa sauti huku tumetabasamu.

(a) Bainisha mambo **matatu** ambayo yanaleta utangamano baina ya vijana wa jamii hii. (alama 3)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

(b) "Kupata elimu pekee hakutoshi kuleta maendeleo." Thibitisha kwa hoja **mbili** kutoka kwenye kifungu. (alama 2)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

(c) Kwa kutoa hoja **nne**, onyesha uhusiano uliopo kati ya nguzo mbalimbali za maendeleo kwa mujibu wa kifungu. (alama 4)

PDF Compressor Free Version

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(d) Eleza mambo **matatu** ambayo yanawachangamsha vijana katika kifungu. (alama 3)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(e) Kauli, "upepo mwanana ulikuwa ukipita na kuzipapasa ngozi zetu," imetumia tamathali gani ya usemi? (alama 1)

..........................................................................................................................

(f) Eleza maana ya, 'tulinoleana bongo' kwa mujibu wa taarifa. (alama 1)

..........................................................................................................................

(g) Andika kisawe cha 'hoja' kwa kurejelea kifungu. (alama 1)

..........................................................................................................................

Teacher.co.ke

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

0774

Teacher.co.ke



**2. UFUPISHO** (Alama 15)

PDF Compressor Free Version

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Binadamu hakuumbwa kuishi katika upweke na kujitenga. Aliumbwa kuwa sehemu ya mfumo wa ushikamano na wenzake. Baadhi ya jamii zinaeleza kwamba Mungu alimuumba mwanamume kwanza na alipoona kwamba anaishi kitwea akamuumbia mwanamke kuwa mshirika wake. Hatua hii ikawa ndio mwanzo wa watu kuishi pamoja kama mke na mume. Yumkini hiki ndicho kiini cha familia. Mshikamano wa familia ni muhimu sana kwa sababu hujenga uhusiano mwema na kushirikiana kimawazo, kikazi na hata zinapozuka haja nyinginezo. Mababu zetu walihitaji sana umoja wa familia. Umoja huo ulifaa mno katika hali mbalimbali. Wakati huo watu walizungukwa na misitu mikubwa ambamo waliishi wanyama wakali kama vile simba, chui na duma. Wanyama hao walikuwa hatari kwa binadamu na hivyo kuwahitaji watu kuungana kuwakabili.

Enzi hizo za mababu pia zilishuhudia uhasama wa kikoo. Koo mbalimbali zilishindana kunyang'anyana mifugo na kung'ang'ania ardhi ili kujijengea himaya zao. Katika hili pia ushirikiano wa karibu ulihitajika ili kujihami dhidi ya uvamizi wowote ule. Kutokuwepo kwa uvamizi kulimaanisha kuwa jamii ilipata utulivu na moyo wa kuendeleza shughuli zao za kila siku ambazo zilikuwa msingi wa maendeleo yao. Watoto nao walipata mazingira salama na tulivu ya kucheza na kukua.

Ushirikiano huu haupo tu katika familia za wanadamu. Tunawaona wanyama wakiwa katika makundi. Wanatembea, kucheza, kula na kulala katika makundi. Makundi haya ni muhimu sana katika maisha ya wanyama mbalimbali. Ulimwengu wa wanyama una adha tele. Adha hizo huwa kisiki kikubwa katika maisha ya wanyama. Zipo hatari za baadhi ya wanyama kuwindwa na kufanywa kitoweo. Mnyama akiwa peke yake huwa windo rahisi kwa wawindaji. Wakiwa katika kundi husaidiana kushika zamu na kutanabahishana hatari ibishapo. Kwa kufanya hivyo huokoleana maisha. Nao wanyama wanaowinda huwa na kibarua kigumu kupata windo wakiwa waenda pweke. Hata simba, mfalme wa msitu, huhitaji kufanya shirika na wenzake ili kuliwahi windo kwa urahisi. Wapo wanyama wala nyama ambao hufa kwa kukosa chakula kwa sababu ya kukaa peke yao.

Hii leo utaona kuwa watu hawashirikiani katika familia tu. Wanashirikiana pia katika mazingira ya shule ambapo wanapokezana maarifa mbalimbali ambayo ni muhimu katika maisha yajayo. Panapokuwa na ushirikiano mzuri kivuno huwa tele kwa mwanafunzi ambaye hujizolea mengi. Hupata elimu ambayo humfungua macho kuona sura tofauti tofauti za ulimwengu, hukuza kipawa chake ambacho anakitumia kwa manufaa yake na ya jamii pana, hujifunza udugu ambao ni muhimu katika kuishi na watu wengine baada ya masomo, na mwanafunzi huweza pia kukomaa kimawazo na kuwa kiungo muhimu cha taifa. Hata hivyo, haya hayaji tu na kumtamia mtu eti kwa sababu amefika na kuishi shuleni kipindi chote cha masomo. Hupatikana kwa mwanafunzi kujenga uthabiti wa fikra na mazoea ya daima kulenga kuwa mtu bora kwa wenzake, awe anawajua au hawajui. Kumbuka kuwa hata wanyama hufanya juhudi kubwa katika kujenga ustadi wao kushirikiana kulipata windo au kukwepa wawindaji.

Taasisi zilizobuniwa kuwa nyenzo za kuendeshea maisha yetu zinajengwa katika misingi hiyo ya familia. Watu huja pamoja na kuunda sheria na kanuni zinazoelekeza utendakazi wao. Bila mpangilio unaohakikisha umoja na ushirikiano miongoni mwa watu, huduma zetu muhimu zingekwama na kutuletea dhiki isiyo mfano. Askari hushirikiana ili kufanikisha kazi yao ya kukomesha uhalifu, walimu hushirikiana kuhakikisha kuwa mwanafunzi amepata elimu ipasayo na ipasavyo, dereva na utingo wake, lazima washirikiane ili kufanikisha safari ya abiria, rais na mawaziri wake hawana budi kushirikiana ili kufanikisha ajenda ya maendeleo.

Ulimwengu wa sasa unahitaji watu wawezao kushirikiana. Wanaposhirikiana, shughuli



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

479
0774

PDF Compressor Free Version

iliyo mbele yao huwa nyepesi na matunda yake huwa ya kufana. Tunaona manufaa ya ushirikiano kwa uwazi zaidi viwandani. Wafanyakazi wa viwandani hugawanya majukumu. Kila mmoja huwa na jambo maalumu analofanya katika mfumo mzima wa uzalishaji bidhaa. Na ndio sababu kiwanda huweza kuzalisha bidhaa nyingi bora na kwa wakati mfupi. Mfano huu wa viwanda unatukumbusha kuwa sawa na viungo vya mwili, sisi wanadamu tuna wajibu maalumu wa kutekeleza kwa kushirikiana na wenzetu. Vinginevyo, kila mmoja akifanya jeuri ya kushika njia yake, uzito wa safari utakuwa mkubwa kwake. Ndio maana wakasema kuwa mtu pweke ni uvundo.

(a) Fupisha ujumbe wa aya **tatu** za kwanza kwa maneno 100. (alama 6)

**Matayarisho**

**Nakala Safi**

Teacher.co.ke

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

(b) Eleza kwa maneno 140, masuala ambayo mwandishi ameibua kuanzia aya ya **nne** hadi ya **sita**. (alama 9)

PDF Compressor Free Version

**Matayarisho**

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

**Nakala safi**

Teacher.co.ke

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

PDF Compressor Free Version

(a) Tofautisha sauti zifuatazo: (alama 2)

(i) /l/ na /r/

..........................................................................................

(ii) /m/ na /b/

..........................................................................................

(b) Bainisha matumizi ya '**ni**' katika sentensi ifuatayo: (alama 1)

Wasaidieni wale, walinisaidia wakati wa shida.

..........................................................................................

(c) Andika neno moja lenye silabi za muundo ufuatao: (alama 1)

Konsonanti + Konsonanti, Irabu + Konsonanti, Konsonanti, Irabu

..........................................................................................

Teacher.co.ke

(d) Tunga sentensi kubainisha kiunganishi kitegemezi. (alama 2)

..........................................................................................

(e) Tumia neno '**vile**' katika sentensi kama:

(i) Kiwakilishi (alama 1)

..........................................................................................

(ii) Kielezi (alama 1)

..........................................................................................

(f) Kutokana na mzizi '**–erevu**' unda:

(i) nomino (alama 1)

..........................................................................................

(ii) kivumishi (alama 1)

..........................................................................................

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

PDF Compressor Free Version

(g) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? (alama 2)

(i) teo ..............................................................................................................

(ii) chanda ........................................................................................................

(h) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo: (alama 3)

Wale wengine watasafiri ughaibuni kwa ndege.

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(i) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya umoja. (alama 1)

Nguo walizouza madukani mwao ziliwavutia watalii.

..........................................................................................................................

(j) Geuza sentensi ifuatayo katika hali yakinishi. (alama 1)

Makuli hawajakuarifu kwamba mizigo hiyo haikuwa yetu?

..........................................................................................................................

(k) Akifisha sentensi ifuatayo. (alama 2)

lo kadio hamadi ndiye mwandishi wa kisiwa chenye tunu

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(l) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi (alama 2)

Mama alimwita Juma na kutaka kujua namna alivyofaulu kuuzima moto huo.

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Teacher.co.ke

(m) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo. (alama 2)

PDF Compressor Free Version

Seremala alilainisha mbao. Seremala alikuwa kiwandani. (Unganisha kuwa sentensi moja inayoanza kwa '**Mbao**' bila kubadilisha maana.)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(n) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 1)

Punde tu <u>alipouliza</u> swali hilo Koru <u>aliingia</u> darasani.

..........................................................................................................................

(o) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea. (alama 1)

Jani ambalo lilipukutika lilipeperushwa na upepo.

..........................................................................................................................

(p) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mstari. (alama 2)

Wakulima hawa wanapanda zao hili daima.

Teacher.co.ke

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(q) Andika sentensi ifuatayo upya ukianzia kwa yambwa tendewa. (alama 1)

Andai alimnywesha babu uji kwa kikombe.

..........................................................................................................................

(r) Tunga sentensi **moja** kuonyesha maana **mbili** za neno **somo**. (alama 2)

..........................................................................................................................

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

(s) Tunga sentensi kubainisha matumizi yafuatayo ya '**kwa**'. (alama 2)

PDF Compressor Free Version

(i) sehemu ya kitu

.......................................................................................................................

(ii) namna

.......................................................................................................................

(t) Tunga sentensi **moja** kubainisha kishazi huru na kishazi kitegemezi. (alama 2)

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

(u) Andika maana **mbili** zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Fundi alimkatia Makaa utepe huo.

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

teacher.co.ke

(v) Zimwi lilizidi kukimbia.
Shujaa aliongeza mwendo kulifikia.
(Unganisha kuwa sentensi moja kwa kutumia neno 'kadiri') (alama 2)

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

(w) Tunga sentensi zifuatazo: (alama 2)

(i) agizi

.......................................................................................................................

(ii) hisishi

.......................................................................................................................

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**4. ISIMUJAMII** (Alama 10)

PDF Compressor Free Version

(a) *Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*

"Karibu, karibu! Keti.
Naam, jitambulishe kwa jopo hili...
Bwana Nuru, ni jambo lipi ambalo linakufanya kuamini kwamba nafasi hii inakuafiki wewe?"

(i) Bainisha sajili ya makala haya. (alama 1)

..................................................................................................................................

(ii) Eleza sifa **nne** za sajili hii kwa kurejelea makala haya. (alama 4)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

Teacher.co.ke

(b) Wewe ni kinara wa chama cha Wanamawasiliano Bora shuleni mwako.

Umepewa jukumu la kuwatangazia wenzako mashindano ya uogeleaji yakiendelea shuleni mwako. Fafanua sifa **tano** za lugha utakayotumia. (alama 5)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**



479
0774
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes